TANGAZO LA SERIKALI Na. 101 la tarehe 16/2/2024

SHERIA YA MIPANGOMIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWAKATIKA ENEO LA IFIGA YA MWAKA 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurasimisha Makazi Yasiyopangwa Katika Eneo la Ifiga ya mwaka 2024.

Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpangokina wa eneo

3. Mpangokina wa eneo lililoainishwa katika Jedwali unaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la urasimishaji lipo ndani ya mipaka ifuatavyo:

"Mpaka unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba E1 yenye majira-nukta 562821MS, 9013520KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Magharibi kwa umbali wa kilomita 0.4 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba E2 yenye majira-nukta 562515MS, 9012998KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Mashariki kwa umbali wa kilomita 1.2 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba E3 yenye majira-nukta 563222MS, 9012165KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Magharibi kwa mbali wa kilomita 0.7 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba E4 yenye majira-nukta 562601MS, 9011866KZ;baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini kufuata mto Kwanana kwa umbali wa kilomita 1.9 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba VMA 619 yenye majira-nukta 561976MS, 9013520KZ;baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Mashariki kwa umbali wa kilomita 1 hadi ulipoanzia."

Dodoma,
29 Desemba, 2023

JERRY WILLIAM SILAA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*